



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**  
**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA**  
**LESENI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA KAMPUNI BAADA YA USAJILI**

Dar es Salaam - 26 Februari, 2024.

Msajili wa Makampuni anapenda kuwataarifu Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa makampuni kwamba baadhi ya makampuni yamekuwa hayatekelezi wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni Taarifa za Mwaka na Mizania (Annual Returns and Audited Accounts) za Kampuni kama Sheria ilivyoelekeza.

Sheria pia, inayataka Makampuni ya Kigeni (Foreign Companies) kuwasilisha Mahesabu yake ya Mwaka kila mwisho wa mwaka (Calendar Year).

Taarifa hizi zinatakiwa kuwasilishwa kwa Msajili wa Makampuni kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (anniversary of incorporation) au tarehe nyingine yoyote ambayo Kampuni itakuwa imeichagua na kumtaarifu Msajili wa Makampuni nae akaridhia. Sharti hili ni kwa mujibu wa Kifungu cha 128 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Msajili wa Makampuni anapenda kuwafahamisha na kuwakumbusha kwamba, kuanzia sasa, Taarifa za Mabadiliko yoyote yanayoletwa na kampuni hayatafanyiwa kazi mpaka Kampuni husika itakapokuwa imewasilisha Taarifa zake za Mwaka.

Taarifa za Mwaka na Mahesabu ya Mwaka kwa kampuni za kigeni (Foreign Companies) husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni, hivyo humuwezesha Msajili wa Makampuni kuwa na taarifa sahihi za Kampuni husika. Makampuni yanahimizwa kuwasilisha Taarifa za Mwaka ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea wakati kampuni inawasilisha taarifa za mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika kampuni.

Kwa usaidizi wa karibu wasiliana nasi kwa simu namba +255(0) 222 212 800.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**